**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

***Barua zote zitumwe kwa*:** **SHULE YA SEKONDARI KWIZU,**
**Simu: +255-714012858** **S.L.P 381,**
**+255-752079001** **SAME.**
**Email:** *kwizusecondary@gmail.com* **09/11/2020.**

Kumb Na: **KWSS/JI/VOLII/2020/21.**

**MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI**

**……………………………………………..**

**S.L.P…………………………………..**

**…………………………………………..**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KWIZU WILAYA YA SAME MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.**

**1. UTANGULIZI**

Ninayo furaha ya kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **KWIZU hongera sana**. Shule hii inapokea wanafunzi wa jinsia zote yaani wavulana na wasichana. Shule ya sekondari **KWIZU** ipo umbali wa **KM45 kutoka** makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.Pia shule ina nafasi za hosteli kwa Wasichana hivyo kwa atakaehitaji kukaa hosteli atafika shuleni kuchukua Fomu ya kujiunga.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11 /01/2021**. Hivyo mwanafunzi unatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe **11/01/2021** bila kukosa.Kinyume na hapo utakuwa umepoteza nafasi yako.

Nakupongeza kwa dhati na nakukaribisha sana kwenye shule yetu ya Kwizu.Utapata likizo mara mbili kwa mwaka na likizo fupi mbili, unaweza ukatakiwa kubaki shuleni wakati wa likizo pale itakapobidi.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### ❖ SARE YA SHULE

**A. WAVULANA**

- Suruali ya kaki jozi mbili zenye linda mbili zisizobana miguuni yaani modo (saizi 18) [kitambaa kimeambatanishwa] kwenye fomu hii.
- Shati jeupe jozi mbili mikono mifupi.
- Viatu vya shule ni vyeusi vya Ngozi na vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeusi jozi mbili
- T-shirt rangi dark bluu yenye nembo ya shule inapatikana shuleni
- Sweta rangi ya kaki mshono wa V shingoni.

**B. WASICHANA**

- Sketi rangi ya kaki jozi mbili [kitambaa kimeambatanishwa] (mshono rinda box) urefu wa soksi inapoanzia ya mguu.
- Shati jeupe jozi mbili mikono mifupi.
- Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na viwe vya ngozi.
- Soksi nyeupe jozi mbili
- T-shirt rangi dark bluu yenye nembo ya shule inapatikana shuleni
- Sweta rangi ya kaki mshono wa V shingoni.
- Rangi ya hijabu (kijuba) ifanane na sare ya shule yaani **nyeupe**

C. **SARE ZA MICHEZO**

- Track suti za rangi ya bluu.
- Bukuta na t-shirt rangi ya njano jozi moja.
- Raba nyeusi jozi moja.

**D. VIFAA VYA DARASANI**

- Daftari kumi, [10] yaani Counter book Quire 2 au Quire 3
- Daftari ndogo kumi (10) kwa ajili ya mazoezi
- Kalamu za buluu na nyeusi zakutosha
- Mkebe wa hesabu [mathematical set].
- Penseli na rula
- Dictionary [Oxford Learner's Dictionary 3rd edition]
- Vifaa vya jikoni yaani sahani na kikombe [sahani ya udongo na sio plastiki].

  NB:
  ***Mwanafunzi asikose Dictionary iliyoelekezwa zaidi ya hapo hatapokelewa.***

**2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote

inayotolewa na wizara ya elimu yenye dhamana ya Elimu nchini na TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

i. Heshima kwa walimu ,viongozi, wafanyakazi na wanajamii wote.
ii. Kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ni lazima.
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
iv. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa
v. Kuzingatia ratiba ya masomo wakati wote.
vi. Kamwe mwanafunzi harusiwi kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha na nwyele ndefu.

## 3. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo darasani/ utoro
iii. Uasherati ,ushoga, ubakaji, ujauzito, kuoa au kuolewa na utoaji mimba.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine, mirungi,na kuberi
v. Kupiga au kupigwa, au kuharibu mali ya shule kwa makusudi
vi. Kudharau bendera ya serikali.
vii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
viii. Kugoma au kuchochea na kuongoza au kushiriki katika kuvuruga amani ya shule au usalama wa watu wengine.
ix. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
x. Kukataa adhabu kwa makusudi.

## 4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

- Fomu ya afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya serikali. Form hii ikabidhiwe kwa mkuu wa shule.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo , fujo na makosa ya jinai
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, Kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa shuleni.

5. ***Tafadhali soma kwa makini maelezo/ magizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KAULI MBIU YA SHULE:** ***ELIMU NI UKOMBOZI. (EDUCATION FOR LIBERATION)***

KARIBU SANA KWIZU SEKONDARI

…………………………………

MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME.**

**SHULE YA SEKONDARI KWIZU, S.L.P 381-SAME.**

**FOMU YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA**

**[Fomu hii ni mkataba kati ya mwanafunzi na shule]**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………………………[Taja majina matatu] nina kubali kujiunga na shule ya Sekondari KWIZU kuanzia mwaka………………………. Hadi mwaka……….. ninaahidi kuwa nitasoma kwa bidii zangu zote na kufuata sheria na kanuni za shule kikamilifu.Sitakuwa tayari kupotosha au kupotoshwa na wenzangu kwa namna yoyote ile yenye kuhatarisha /kuvua hadhi ya uwanafunzi wangu.

Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………………… Tarehe…………….

**SEHEMU YA MZAZI / MLEZI**

Mimi ……………………………………………………………………(taja majina yako matatu) mzazi/ mlezi wa…………………………………………Nimekubali mtoto wangu ajiunge na shule ya Sekondari Kwizu na nina ahidi kwa dhati kabisa kutimiza majukumu yote yatakayo nihusu kama mzazi/mlezi kamwe sitakuwa kikwazo katika tendo la kujifunza kwake shuleni.

Alizaliwa tarehe………………………….. mwezi………………… mwaka…………………

Mahali Alipozaliwa kitongoji cha…………………….. Kijiji cha……………………. kata ya…………………

Kazi ya baba/ mlezi wakiume………………….. kazi ya mama/ mlezi kike…………………….

Ndugu wawili wa karibu ambao wanaweza kukusaidia wakati ukiwa nashida au wakati wa dharura.

1. Jina………………………………………………………Anuani…………………….......
   Namba ya simu…………………………. Uhusiano……………………………………
2. Jina……………………………………………………… Anuani………………………….
   Namba ya simu …………………………. Uhusiano…………………………………………

Ripoti ya maendeleo yake itatumwa kwa……………………………………………………..
kwa kutumia anuani ifutayo……………………… Namba ya simu……………………….

Sahihi ya mzazi / mlezi ………………………………………………

THE PRESIDENT'S OFFICE-RALG
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

KWIZU SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 381,
**SAME.**
DATE:…………………………

TO MEDICAL OFFICER
…………………………….
…………………………….
……………………………

PART A
MR/MRS/MISS …………………………………….……….. please examine the student named …………………………………………………………………….. as her/ his physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories;

1. Haemoglobin ……………………………………………………………………………..
2. P.V. Bleeding …………………………………………………………………………….
3. Eye sight …………………………………………………………………………………
4. Blood pressure …………………………………………………………………………..
5. Urine for sugar …………………………………………………………………………..
6. Stool for examination ……………………………………………………………………
7. Asthma ……………………………………………………………………………….
8. Skin diseases ……………………………………………………………………………
9. Leprosy ………………………………………………………………………………..
10. Epilepsy ………………………………………………………………………………..
11. Any deformity …………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis ………………………………………………………………..
13. Neurosis ………………………………………………………………………………..
14. Venereal disease ……………………………………………………………………….
15. Other serious diseases ………………………………………………………………….
16. Pregnancy ………………………………………………………………………………

Thank you
………………………
HEADMASTER

PART B
MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by Government Medical officer

1. I have examined the above-named student and find that He/ She is physically **fit/ unfit** and mentally **fit/ unfit** for full time schooling.
2. OTHE COMMENTS
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………

   Date: …………………… Name and Signature: ……………………………………………….

   DESIGNATION ………………………………. OFFICIAL STAMP: …………………………..